## Maswali

1. Mbona Mungu alipea Yesu zawadi?
2. Mbona Mungu alimjaribu Yesu?
3. Mawazo ya Yesu yalitoka wapi?
4. Mbona Biblia inazungumzia dhambi kama ni mtu?
5. Ibilisi ni nini?
6. Mbona Yesu hakugeuza mawe yakawa mkate?
7. Mbona Yesu hakuruka kutoka kwa hekalu?
8. Mbona Yesu hakukuwa mfalme?
9. Alifanyaje kupigana na jaribio?
10. Tunajuaje kwamba mawazo yetu hayampendezi Mungu?

## Majibu

1. Kwa sababu alimpenda na alitaka Yesu aonyeshe watu kwamba yeye ni mwana wa Mungu.
2. Kwa sababu Mungu alitaka kujua kama Yesu atatumia uwezo wa Mungu kufanya mambo yake au ya Mungu.
3. Mawazo ya Yesu yalitoka moyoni mwake. Ni mambo aliyoyafikiria na alitaka kuyafanya.
4. Biblia inazungumzia dhambi kama ni mtu ndio sisi tupigane nayo na tuisukume mbali.
5. Ibilisi ni mawazo yetu ya dhambi. Si mtu, ni mawazo na tamaa yetu inayotoka moyoni mwetu.
6. Kwa sababu angetumia nguvu za Mungu kwa uchoyo.
7. Yesu hakuruka kutoka hekaluni kwa sababu Mungu hakutaka atumie njia hii kuonyesha yeye ni mwana wa Mungu.
8. Yesu hakukuwa Mfalme kwa sababu hii ilikuwa mpango wa Mungu ya wakati ujao- sio saa hizo. Alitaka Yesu aonyeshe mfano mzuri kama mtumishi.
9. Yesu alitumia neno la Mungu kuhepa mawazo yasiyo ya kimungu (ibilisi) Kutoka moyoni mwake. Alibadilisha hayo mawazo mabaya na neno la Mungu.
10. Tukiendelea kusoma neno la \Mungu tutajua ni nini inamfurahisha Mungu. Tutafahamu kama mawazo yetu ni kama ya Mungu.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 2**

# 32 Majaribu ya Yesu

## Marejeo

Mathayo 3:16 mpaka Mathayo 4:11

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Yesu alijaribiwa tu kama sisi lakini hakushindwa, hakukubali hayo mawazo yake.

## Maneno maalum


1. Yesu + Batizwa + zawadi + roho mtakatifu + jaribu.
2. Siku arobaini + hakuna chakula + mawazo mengi + saidia wengine + moyo wake + si Mungu.
3. Pigana + majaribu + mawaso yake + dhambi + ibilisi + kutoka moyoni.
4. Njaa + mawe + mkate + hakikisha + mwana wa Mungu + saidia watu kuamini + maneno ya Mungu + kumbuka.
5. Jaribio + kitu cha ajabu + mwana wa Mungu + ruka + kutoka kwa hekalu + malaika +hutaumia + si njia ya Mungu.
6. Jaribio + nguvu + mfalme + dhania + mlima + mfalme mzuri + baadaye + si saa hii + mtumishi + mfano + funza + hudumu + pigana na jaribio + neno la Mungu.
7. Choka + faulu + mawazo + Mungu kwanza + njia ya Mungu + mawazo yalimuacha + rudisha hali + mawazo ya kimungu + futa + kushindana na Mungu + jaza mawazo na Mungu.

**32.1** Baada ya Yesu kubatizwa, Mungu alimpa zawadi. Alimpa nguvu zake, Roho Mtakatifu. Hii ilimaanisha Yesu alikuwa na uwezo wa kufanya chochote alichotaka. Mungu alitaka kujua vile Yesu angetumia huo uwezo. Angeutumia kwa yeye mwenyewe? Angeitumia kupata chochote alichotaka? Ama angeitumia kufanya mambo ya kuonyesha yeye ni mwana wa Mungu. Mungu alijua kwamba Yesu alitakiwa awe na wakati wa kuamua afanye nini kwa hivyo Mungu alimpeleka jangwani kumjaribu.

**32.2** Yesu alikaa jangwani kwa siku arobaini bila chakula. Wakati huu wote mawazo yalimjaa kichwani mwake juu ya kutumia uwezo wake. Angejifanyia mambo mengi na hata kusaidia watu wengine. Aliwaza vile angewabadilisha watu wamrudie Mungu- lakini haya yalitoka moyoni mwake sio kwa Mungu.

**32.3** Kwa sababu ilikuwa mawazo yake. Yesu alijaribu kabisa kushindana nayo. Mungu anajua vile ni vigumu kushindana na nguvu ya dhambi. Anaitambulisha kama ni mtu na huwa anatusaidia kupigana nayo ili teepukane nayo. Haya mawazo ya ndani kwa wakati mwingine huitwa ibilisi. Sio mtu lakini huwa mawazo na tamaa ya moyo wa mtu.

**32.4** Yesu alikuwa na njaa kwa siku 40. Aliona mawe chini na akailinganisha na mikate. Alijua anauwezo wa kubadilisha mawe iwe mikate. Kama angefanya hivyo angekuwa ametumia nguvu za Mungu kwa yeye mwenyewe tu. Lakini Mungu alikuwa amempa hizo nguvu ili azitumie kuonyesha watu kwamba yeye ni mwana wa Mungu. Ilikuwa kusaidia watu waamini maneno yake.



Huko jangwani hakukuwa na mtu wakuona vile angetumia huo uwezo kwa miiujiza ndio watu waamini Mungu. Hapo alikumbuka maneno ya Mungu na akayatumia kuenenda kwa njia za Mungu (soma maneno yenye Yesu alisema – Mathayo 4:4).

**32.5** Halafu Yesu alijaribiwa kufanya jambo la ajabu kuonyesha kila mtu kwamba yeye ni mwana wa Mungu. Alifikiri kwamba angeruka kutoka kwa Hekalu la Yerusalemu kwa sababu Zaburi 91 inasema Mungu atatuma malaika wamshikilie asiumie. Lakini hii sio njia yenye Mungu alitaka aonyeshe yeye ni mwana wake. Mara tena Yesu akaamua kuenenda kwa njia za Mungu tena akatumia neno la Mungu ili afaulu (soma alichosema Mathayo 4:7).

**32.6** Tena Yesu alijaribiwa kutumia uwezo wake ili awe Mfalme na alete amani ulimwenguni. Alijiona ako juu ya mlima na ameona mataifa ya ulimwengu wote. Aliona huo uwezo wa kutawala na angekuwa mfalme mzuri. Lakini hii ilikuwa ni mpango wa Mungu wa baadaye, sio saa hizo. Kwanza alitaka Yesu awe mtumishi si mfalme. Hapa watu wangeona Yesu kama mfano wakufuata vile wanaweza kumtumikia Mungu kwa maisha yao. Tena hapa Yesu anafaulu kuhepa majaribu kwa kutumia neno la Mungu. (soma alichosemaa Mathayo 4:10).

**32.7** Baada ya haya yote Yesu alikuwa amechoka. Alikuwa amefaulu kupigana na mawazo yake. Aliakikisha kwamba Mungu anakuja kwanza. Alikuwa ameamua kuenenda kwa njia za Mungu. Kwa hivyo hayo mawazo yalimtoka-alikuwa amezibadilisha na mawazo ya kimungu. Ndiyo njia ya pekee ya kupigana na majaribu – kwa kufutilia mbali mambo ya akili zetu zisizo za Mungu na kuyajaza na mambo ya kimungu.